**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAS – UTAWALA BORA KAPT (MST) GEORGE HURUMA MKUCHIKA (MB), WAKATI AKIFUNGUA MKUTANO WA WADAU KUHUSU MPANGO KAZI WA KUENDESHA SHUGHULI ZA SERIKALI KWA UWAZI (OGP) WA AWAMU YA PILI KATIKA UKUMBI WA MAKUMBUSHO, MEI 09, 2014**

**Bibi Susan Mlawi, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - Ikulu na Mwenyekiti wa Mkutano huu,**

**Bw. Rajani Rakesh, Mkurugenzi wa TWAWEZA na Mwakilishi wa Asasi Zisizo za Kiserikali,**

**Ndugu Wadau wa Mpango Kazi wa Kuendesha Shuhguli za Serikali kwa Uwazi (OGP),**

**Mabibi na Mabwana,**

Awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa kunialika kuwa mgeni rasmi katika ufunguzi wa mkutano huu muhimu wa Wadau wa Uendeshaji wa Shughuli za Serikali kwa Uwazi (Open Government Partnership – OGP) utakaojadili utekelezaji wa awamu ya pili ya Mpango Kazi wa OGP. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Wajumbe kwa kuitikia wito wa kuhudhuria mkutano huu kwani kufika kwenu ndio mafanikio yake. Vile vile, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza

Viongozi na Wadau wote kwa kazi nzuri ambazo mmeendelea kuzifanya katika kutekeleza malengo yake.

Tangu Serikali ilipojiunga na mpango huu wa Kimataifa mwezi Septemba 2011, tumendelea kushuhudia mabadiliko ya kuongezeka kwa uwazi na uwajibikaji katika sekta mbalimbali. Mabadiliko hayo yanaonekana katika utoaji wa huduma, ushirikishwaji wa wananchi katika maamuzi na mipango ya Serikali, mapambano dhidi ya rushwa na uendelezaji wa masuala ya teknolojia nchini. Hali hiyo ya utendaji wa pamoja inadhihirisha uwepo wa dhana ya ushirikishwaji katika uendeshaji wa mpango wa OGP.

**Ndugu Washiriki**,

Mpango Kazi wa Awamu ya Kwanza wa OGP umetekelezwa kwa ufanisi ambapo mfumo wa takwimu nchini umedadavuliwa vyema na mipango ya maandalizi ya taratibu za matumizi ya takwimu mbalimbali inaendelea kuwekwa sawa ili kuongeza uwazi zaidi na pia matumizi ya takwimu hizo katika kuandaa mipango ya maendeleo ya nchi. Aidha, nimeelezwa kwamba ufanisi wa utekelezaji wa mpango huu unaendelea kuimarisha mipango mingine ya utawala bora nchini. Vilevile, tovuti katika sekta za Umma zimeboreshwa na taarifa mbalimbali muhimu zimewekwa zikiwa tayari kutumika na wananchi na wadau wengine.

Bajeti za serikali na sera mbalimbali zimewekwa wazi na wananchi

wameanza kupata fursa ya kuzisoma katika lugha rahisi na kuchambua. Ni katika kipindi hicho ambacho tovuti ya "wananchi", tovuti ya "nifanyeje" na "portal" ya serikali zilianzishwa ambapo taasisi za umma zitakuwa tayari kuweka taarifa muhimu kwa wananchi, hali ambayo inatimiza malengo ya mpango wa OGP ya kuongeza uwazi, uwajibikaji na ushirikishwaji wa wananchi katika shughuli za nchi.

**Ndugu Washiriki**,

Ni ukweli usiopingika kwamba kila jambo jema halikosi kasoro. Pamoja na mafaniko yaliyopatikana pia kumekuwepo na changamoto mbalimbali. Utekelezaji wa mpango wa OGP haujaweza kupelekwa katika ngazi za Mikoa, Wilaya, Kata na Vijijini. Kwa kuzingatia umuhimu wa mpango huu kuna kila sababu ya kuupeleka huko. Pia, katika hatua za utekelezaji wa mpango huu, rasilimali fedha kwa kiwango fulani hazikuweza kupatikana kulingana na mipango iliyowekwa. Aidha, kumekuwepo na ushiriki mdogo wa Asasi Zisizo za Kiserikali katika kutekeleza mpango huu. Asasi hizo ni Wadau muhimu ambao ushiriki wao unakamilisha na kuendeleza malengo ya mpango wa OGP.

**Ndugu Washiriki,**

Utekelezaji wa Mpango Kazi wa Awamu ya Kwanza wa OGP kwa mwaka wa fedha 2011/12 hadi 2012/13 bado unaendelea. Hatua iliyopo sasa ni kuandaa Mpango Kazi wa Awamu ya Pili wa miaka

miwili (2) utakaoanza kutekelezwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15 hadi 2015/16.

Utekelezaji wa Mpango wa Awamu ya Pili utazingatia mafanikio na changamoto za Awamu ya Kwanza. Mafanikio hayo yataboreshwa na kuendelezwa na changamoto zote kutafutiwa ufumbuzi ili malengo ya mpango huo yatimizwe. Mpango Kazi wa awamu ya kwanza ulitoa kipaumbele kwa sekta za elimu, maji na afya. Mpango Kazi wa awamu ya pili utaendeleza vipaumbele vya sekta za elimu, maji na afya na pia zimeongezwa sekta za ardhi na madini. Sekta hizi zina umuhimu mkubwa kwa wananchi katika nyanja za kijamii, kiuchumi na kisiasa katika kujenga utawala bora nchini.

**Ndugu Washiriki,**

Kazi kubwa tuliyonayo leo hii ni kuchambua mapendekezo tuliyopewa na Serikali kuhusu maeneo ya kutekelezwa katika Mpango wa OGP awamu ya pili. Mfumo uliotumika kupitisha Mpango Kazi wa awamu ya kwanza ndio unaotumika katika awamu hii. Hivyo, mnalo jukumu kubwa la kuboresha mapendekezo haya pale mtakapoona inafaa. Tunahitaji Mpango Kazi wa awamu ya pili ulete matokeo makubwa. Michango yenu ni muhimu sana katika kufikia malengo yanayokusudiwa. Nimejulishwa kwamba baada ya ufunguzi wa mkutano huu washiriki mtajipanga katika vikundi na kupewa maswali ambayo mtayajadili na majawabu mtakayotoa yatatumika katika kuboresha utekelezaji wa Mpango wa OGP

awamu ya pili.

**Ndugu Washiriki,**

Mpango huu wa OGP unatumika kikamilifu katika kuendeleza mipango mingine ya serikali ya kujenga na kuendeleza utawala bora nchini. Hivyo, inashauriwa kwamba mafanikio yaliyopatikana katika awamu ya kwanza yawe ni chachu katika awamu ya pili. Ufanisi uwe mkubwa kwani kwa kufanya hivyo utoaji wa huduma kwa wananchi utongezeka na kupatikana kwa maendeleo makubwa. Aidha, utekelezaji wa OGP awamu ya pili unahitaji ushirikiano mkubwa wa wadau wote. Wadau wa Sekta binafsi na Asasi Zisizo za Kiserikali wanatanabahishwa kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa mpango huu. Hivyo, suala la kutaka kuwepo kwa mashirikiano ya pamoja halina mjadala. Ni wakati mwafaka sasa wa kuboresha Mpango Kazi wa OGP kwa kuwa na ushirikiano wa pamoja.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Jakaya Mrisho Kikwete amewahi kuelezea thamani ya Mpango wa Uendeshaji wa Shughuli za Serikali kwa Uwazi (OGP) akisema, namnukuu “ukweli, uwazi na uwajibikaji ni muhimu kwa Serikali na wananchi kwa sababu serikali inapokuwa wazi wananchi wanajua kitu gani kinaendelea na wanaweza kuiwajibisha na hivyo serikali inayo mambo mengi ya kufanya” mwisho wa kunukuu.

**Ndugu Washiriki,**

Napenda kutumia nafasi hii kutoa msisitizo kuwa siku ya leo itumike vizuri katika kutoa maoni ili tuwe na Mpango wa OGP utakao tekelezeka na hatimaye kuwa chachu ya kuleta maendeleo kwa wananchi. Rekebisheni Mpango Kazi huu pale mtakapoona inafaa ili mwisho wa siku

ionekane ni kazi mliyoifanya wenyewe na ambayo mtawajibika moja kwa moja. Nyinyi kama Wadau mnatakiwa kuwa na ratiba za vikao vya pamoja vya kufuatilia utekelezaji wa Mpango Kazi wa OGP. Umma uelimishwe kuhusu utekelezaji na umuhimu wa mpango huu kwa jamii.

Jadilini Mpango huu kwa uhuru. Msisitizo uwekwe kwenye mambo yote yatakayoleta maendeleo ya haraka kwa wananchi. Hasa kujenga uwazi na uwajibikaji, ushirikishwaji wa wananchi katika shughuli za Serikali, kusimamia mapambano dhidi ya rushwa na maendeleo ya technolojia. Ni matarajio ya Serikali kwamba maoni yenu yatakuwa ya kujenga na kuimarisha utendaji wa Serikali. Nami kama Mratibu Mkuu wa masuala ya Utawala Bora chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania naahidi kuwa nanyi bega kwa bega katika utekelezaji wa awamu ya pili ya Mpango Kazi wa OGP.

Kwa haya machache napenda kutamka kwamba sasa Mkutano wa

Wadau wa kupata Maoni ya Mpango Kazi wa awamu ya pili ya OGP umefunguliwa rasmi.  Nawatakia kazi njema na mafanikio katika kazi hii.

**AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA**